BARAZA LA WAWAKILISHI
ZANZIBAR

Simu ya Upepo: Baraza
Nambari ya Simu:2230234/5
Tele Fax. Nam. (024)2230215

SANDUKU LA BARUA 902,
ZANZIBAR

RIPOTI YA KAMATI YA KUCHUNGUZA NA KUDHIBITI HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA (P.A.C) YA BARAZA LA WAWAKILISHI, ZANZIBAR KWA MWAKA WA FEDHA 2007/2008.

SEHEMU YA KWANZA:
UTANGULIZI

1.1 NGUVU ZA KISHERIA ZA KAMATI:

Kamati ya kuchunguza Hesabu za Serikali na Mashirika imeundwa chini ya kanuni 113 ya Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2009.

1.2 MAJUKUMU YA KAZI ZA KAMATI YA KUCHUNGUZA HESABU ZA SERIKALI NA MASHIRIKA:

Kwa mujibu wa Kanuni ya 113 ya Baraza la Wawakilishi toleo la 2009, Kamati ya P.A.C inatekeleza majukumu yake kama ifutavyo:

- Kuchunguza na kutoa taarifa juu ya hesabu za mwaka za matumizi ya fedha za Serikali na Mashirika yake na hesabu nyengine zozote zitakazowasilishwa mbele ya Baraza kupitia ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.
- Kuchambua na kutafakari ripoti yeyote ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali pale ambapo Rais aliagiza ukaguzi huo ufanywe.
- Kuchunguza kwa njia yeyote inayoona mambo yote yanayohusu hesabu za Serikali na asasi zake.
- Kutoa Ripoti yake baada ya kufanya uchunguzi kuhusiana na matumizi ya ziada ya fedha iliyotolewa kwa mwaka wa fedha unaohusika.
- Katika kufanya kazi zakeKamati ya PAC itakuwa na wajibu wa kuchunguza kama:
  Fedha zilizooneshwa katika makadirio ya Matumizi ya Serikali na Mashirika yake zimetumika kama iliyvo kubaliwa na matumizi yalikuwa chini ya mamlaka iliyohusika na Matumizi yaliyofanywa yalizingatia thamani halisi ya fedha.

1.3 UPEO WA KAZI:

Kamati ya PAC katika kutekeleza kazi zake kwa mwaka huu wa fedha 2009/2010 imeweza kuipitia Ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali za mwaka 2007/2008. Hata hivyo kutokana na muda kuwa mdogo sana, Kamati imeshindwa kufutialia baadhi ya hoja za Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali zinazohusu Miradi, Kamati inatarajia kuendelea na kazi hiyo katika kipindi kijacho cha kazi za Kamati.

1.4 MAMBO YALIYOBAINIKA KATIKA UKAGUZI WA KAMATI:

Kamati baada ya kufuatilia hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka wa 2007/2008 pamoja na mambo mengine, imebaini mambo yafuatayo:

Matumizi yasiyo na vielelezo:

Ukaguzi wa Kamati umebaini kuwa Idara na Taasisi zifuatazo zimefanya matumizi ambayo hayakuwa na vielelezo:-

- Kikosi cha Valantia, Tsh. 12,733,450/-.
- Wizara ya Afya, Tsh. 61,187,500/-.
- Shirika la Utalii, USD 12,545.

Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi:
Ukaguzi umebaini kuwa jumla ya Tsh.26,963,500/- zimetumika bila ya kuwepo kumbukumbu na vitabu vya kuwekea kumbukumbu za hesabu katika Shirika la Huduma za Maktaba.

Upotevu wa Mishahara:
Ukaguzi umegundua kuwa, Kikosi cha Zimamoto na Uokozi kimepoteza Tsh. 23,240,556/- za mishahara ya wafanyakazi wake.

Vile vile kwa upande wa Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii, Pemba katika kitengo cha Micheweni Cottage, kimepoteza mishahara ya wafanyakazi wake yenye thamani ya Tsh. 4,878,256.

Madeni ya Wizara na Taasisi za Serikali:
Ukaguzi umebaini kuwa Wizara na Taasisi zifuatazo zinakabiliwa na madeni ya muda mrefu:-

- Hoteli ya Bwawani inadai baada ya kutoa huduma jumla ya Tsh. 21,779,600/- na USD 1369.
- Sauti ya Tanzania Zanzibar inadai baada ya kutoa huduma jumla ya Tsh. 18,065,000/-.
- Mfuko wa Kujitegemea, imekopesha watu mbali mbali jumla ya Tsh. 10,846,500/-.
- Idara ya Ardhi na Usajili inadai deni la kodi ya Ardhi kwa wawekezaji jumla ya USD 1,554,091.80 na deni la kodi ya nyumba ni Tsh. 175,800,145/-.
- Karakana ya Matrekta, wanadai jumla ya Tsh. 112,446,904.20/-
- Wizara ya Afya, Pemba inadaiwa na wafanya biashara na Taasisi za Serikali na watu binafsi jumla ya Tsh. 144,448,351/-
- Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi, Pemba inadai kwa watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh.36,951,580/- na USD 67,775.
- Mamlaka ya Maji, Pemba inadai kwa wateja wake, watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh.4,493,000/-
- Jeshi la Kujenga Uchumi, Pemba, inadaiwa na wafanya biashara na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh.38,767,600/- na inawadai watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh. 40,723,788/-
- Baraza la Mji, Chake Chake inadaiwa na dula la City Furniture, Dar es Salaam jumla ya Tsh. 14,832,000/-
- Shirika la Bandari linawadai watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh. 2,417,138,133.64/-
- Shirika la Meli na Uwakala, linawadai watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh. 57,036,411.85/-
- Shirika la Biashara ya Magari linawadai watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh.61,222,654.60/-
- Shirika la Utalii linawadai watu binafsi na Taasisi za Serikali jumla ya Tsh. 4,525,000 na USD 19,850 aidha, linadaiwa na Taasisi za watu binafsi na za Serikali jumla ya Tsh. 104,530,793.52/-.

1.5 MUUNDO WA RIPOTI:

Ripoti inatoa taarifa za hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka 2007/2008 ambapo itakuwa imegawika sehemu kuu tatu. Sehemu ya kwanza ni utangulizi

unaonyesha nguvu za sheria za kuundwa kwa Kamati ya PAC, Majukumu yake pamoja na majina ya wajumbe wa Kamati. Sehemu ya pili inatoa ufafanuzi juu ya hoja mbali mbali za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kama zilivyoainishwa katika kitabu cha Mkaguzi wa Hesabu. Sehemu ya tatu itakuwa ni hitimisho ambapo kutakuwa na mapendekezo ya Kamati kwa Baraza.

1.6 WAJUMBE WA KAMATI:

Kamati ya kuchunguza hesabu za Serikali na Mashirika kwa mwaka 2009/20010 iliundwa na wajumbe 10 na makatibu 2.Wajumbe wenyewe ni kama wafuatao:-

1.	Mhe.Fatma Abdulhabib Fereji	Mwenyekiti
2.	Mhe.Omar Ali Shehe	Makamo Mwenyekiti
3.	Mhe.Abbass Juma Muhunzi	Mjumbe
4.	Mhe.Ahmed Nassor Mazurui	Mjumbe
5.	Mhe.Ali Mohamed Bakar	Mjumbe
6.	Mhe.Anaclet Thobias Mkungila	Mjumbe
7.	Mhe.Hija Hassan Hija	Mjumbe
8.	Mhe.Mkongwe Nassor Juma	Mjumbe
9.	Mhe.Said Ali Mbarouk	Mjumbe
10	Mhe.Thuwaybah Edington Kisasi	Mjumbe
11	Ndg.Shemsa Maabad Mohamed	Katibu
12	Ndg.Othman Ali Haji	Katibu

SEHEMU YA PILI:
UFAFANUZI WA HOJA ZA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KWA TAASISI ZA UNGUJA:

2.0 WIZARA YA FEDHA NA UCHUMI:

Hoja nam. 1.1 kuhusu vifaa ambavyo havikuingizwa katika Daftari la Ghalani (Store Ledger) vyenye thamani ya Tsh. 9,062,800/-

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli wakati wa ukaguzi, vifaa hivyo vilikuwa havijaingizwa katika daftari la vifaa, ingawaje wakati wa kazi za Kamati, vifaa hivyo vilikuwa tayari vimeshainginzwa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imekemea tabia ya Wizara kucheleweshe kuingiza vifaa katika daftari la Ghalani kwa wakati. Hata hivyo, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 1.2 kuhusu malipo yasiyokuwa na stakabadhi, Tsh. 2,133,622/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Hati namba C.23/12/2007 yenye thamani ya Tsh. 1.077,382/- tayari imeshapatikana huku Wizara imeshindwa kuwasilisha mbele ya Kamati hati namba C.12/9/2007 na kuwasilisha “pay slip” ya risiti hiyo.

MAONI YA KAMATI.
Pamoja na kukosekana kwa risiti hiyo, Kamati imejiridhisha kufanyika kwa malipo hayo kupitia pay in slip hiyo. Hata hivyo, Kamati imeitaka Wizara kuhakikisha inapata risiti za kuhalalisha malipo husika.

2.1 WIZARA YA NCHI (AR) TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA S.M.Z.

2.1.1 KIKOSI CHA VALANTIA:
Hoja nam. 5.1 kuhusu Matumizi yenye thamanai ya Tsh. 24,733,450/- yaliyofanyika bila ya Stakabadhi.

MAPITIO YA KAMATI:
Stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi, ziliwasilishwa mbele ya Kamati. Hata hivyo, Kamati haikutosheka na stakabadhi aliyolipwa Mtoni Motors Agency, yenye thamani ya Tsh. 12,733,450 yenye hundi namba 284392.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inahitaji document nyengine zaidi zinazoonyesha ufafanuzi wa malipo hayo.

2.1.2 KIKOSI CHA ZIMA MOTO NA UOKOZI
Hoja Nam 6.1 upotevu wa mishahara wa jumla ya Tshs 23,240,556 ulioliotokea katika kikosi cha Zimamoto na Uokozi.

MAPITIO YA KAMATI
Kamati imeelezwa kuwa suala hilo kweli limetokea na kesi iko Mahkamani.

MAONI YA KAMATI
Kamati imeliacha suala hili lishughulikiwe katika ngazi ya mahkama kwanza.

3.0 WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI.

Hoja Nam. 31.1 kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka.
Baada ya kufunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka za Wizara husika, yafuatayo yamegundulika:

Kushindwa kupatikana kwa idadi halisi ya fedha na mali zilizopatikana kutoka kwa wahisani kwa vile hazikuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka.

MAPITIO YA KAMATI:
Kuhusu kushindwa kupatikana kwa idadi halisi ya Fedha za Wahisani wa Maendeleo kwa baadhi ya Miradi, Kamati imefahamishwa kwamba, Wizara haipewi fedha hizo moja kwa moja. Fedha hizo huratibiwa na kufanya malipo wao wenyewe kwa kuwalipa Wakandarasi na Washauri moja kwa moja kupitia Account zao, Wizara inachopokea ni hati za malipo na baada ya kuthibitishwa uhalali wa malipo huwasilishwa kwa wahusika kwa hatua zao. Aidha, Kamati imefahamishwa kwamba, hati za malipo zenye thamani ya Tsh. 11,180,511,820 kwa mwaka 2007/2008 zimelipwa kwa Makampuni SSMEHTA, BLACK & VEATCH, SPENCON, KUNDANSINGH na SMEC.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na kupokea majibu haya, Kamati inashauri Afisi ya Mdhibiti iarifiwe mapema ili hoja ambazo majibu yake yapo wazi, zisijitokeze katika ripoti ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu.

Kukosekana kwa nyaraka za uingizaji wa fedha ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi.
Ukaguzi ulibaini kwamba Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi imepokea nyaraka za taarifa za uingizaji wa fedha kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi, lakini nyaraka hizo hazikupatikana kwa ukaguzi. Nyaraka za kazi za kawaida zina thamani ya Tsh. 253,419,315 na kwa kazi za maendeleo ni Tsh. 650,000,000/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Nyaraka zilizokosekana wakati wa ukaguzi ziliwasilishwa mbele ya Kamati ingawa bado hazijakaguliwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeagiza Wizara izipeleke nyaraka hizo kwa Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu ili azikague na hatimae, Wizara iijuilishe Kamati kuhusu utekelezaji wa agizo hili.

3.1 IDARA YA MIPANGO NA UENDESHAJI:

Hoja Nam. 30.1
Hoja hii ina sehemu mbili, Kuhusu Mdhibiti wa Ndani (Internal Control), kwamba Wizara haina Kamati ya Ukaguzi wa hesabu (Audit Committee), vile vile ukaguzi ulibaini kwamba, hakuna Bodi ya Zabuni iliyoundwa.

MAPITIO YA KAMATI.
Ni kweli kwamba, hapo awali Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za ndani (Audit Committee) haikuwepo, ingawa Kamati imefahamishwa kwamba Kamati hiyo sasa imeshaundwa na kuzinduliwa mwaka 2008 na hivi sasa inaandaa ripoti ya 2 na kuiwasilisha kwa Katibu Mkuu wa Wizara.

Kuhusu Bodi ya Zabuni, Kamati imefahamishwa kwamba, hivi sasa Bodi hiyo ipo na inafanya kazi zake.

MAONI YA KAMATI.
Kamati imepongeza kuanzishwa ka Kamati ya Ukaguzi wa Hesabu za ndani na Bodi ya Zabuni na kuitaka Wizara iziwezeshe kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

3.1.2 IDARA YA ANGA:

Hoja Nam. 30.2
Kuhusu Madeni ya Utuaji Ndege (Landing Charges) ya Tsh. 290,799,944/- na USD 23,028 kutoka kwa Mashirika mbali mbali bado hayajalipwa.

MAPITIO YA KAMATI.
Kamati imefahamishwa kwamba, Asilimia tisiini (90%) ya madeni hayo imeshalipwa. Hata hivyo, Kamati imefahamishwa kwamba, kutokana na mfumo wa biashara yenyewe madeni hayo yataendelea, kwa vile biashara inafanywa mwanzo halafu malipo hulipwa baadae.

MAONI YA KAMATI
Kwa kuzingatia mfumo wa biashara husika, Kamati inaelekeza juhudi za kudai madeni hayo iendelee na Wizara ihakikishe kwamba wadaiwa wanalipa madeni yao kwa wakati.

4.0 WIZARA YA UTALII, BIASHARA NA UWEKEZAJI. WIZARA YA UTALII, BIASHARA NA UWEKEZAJI.

Hoja Nam. 36.1 kuhusu malipo yasiyokuwa na vielelezo vya thamani ya Tsh. 999, 360/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi, viliwasilishwa mbele ya Kamati vikiwa vimekamilika.

MAONI YA KAMATI.
Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja namba 36.2 kuhusu vifaa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la ghalani (Store Ledger) vyenye thamani ya Tsh. 250,000/-

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli wakati wa ukaguzi, vifaa hivyo vilikuwa havikuingizwa katika daftari, ambapo wakati wa kazi za Kamati ilikutia vifaa hivyo vimeshaingizwa na Kamati imelikaguliwa daftari hilo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaelekeza kwamba, baada ya kurekebishwa kilichoonekana kuwa ni upungufu na Mdhibiti, Taasisi husika ichukue hatua za kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na hatimae taarifa zifikishwe kwa Kamati.

Hoja namba 36.3 kuhusu hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi zenye thamani ya Tshs 86.392/=

Mapitio ya Kamati:
Hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi zimewasilishwa na kukaguliwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI.
Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

4.1 HOTELI YA BWAWANI:

Hoja nam.39.1 Kuhusu udhaifu wa udhibiti wa ndani (Internal Control) kwa baadhi ya taratibu za fedha zinazotumika katika Hoteli hiyo, ambazo ni Kukosekana Wakaguzi wa ndani (Internal Audtors) watakaousaidia uongozi wa Hoteli kwa kutoa ripoti; Kutotayarishwa kwa ripoti ya mwaka ya fedha (Financial Account) ambayo itatoa picha halisi ya mahesabu ya Hoteli kwa Serikali; Kutokuwepo kwa daftari kamilifu la samani linalohusiana na uwekaji wa kumbukumbu za samani (Fixed Asset Register).

MAPITIO YA KAMATI.
Ni kweli Hoteli haina Mkaguzi wake wa Ndani isipokuwa inategemea Wakaguzi wa ndani wa Wizara ya Utalii, Biashara na Uwekezaji. Pia Hoteli imekiri makosa yaliyojitokeza kuhusiana na hoja ya Mdibiti inayohusu kutotayarisha ripoti ya mwaka ya fedha na kwamba sasa wamesharekebisha. Kuhusu Daftari la Kumbu kumbu za samani, Hoteli bado haina Daftari hilo isipokuwa imeweka rikodi ya samani hizo katika utaratibu ambao hata Kamati haikuridhika nao.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishwa na hatua zilizochukuliwa na Uongozi wa Hoteli kuhusiana na majibu ya Hoja ya Mdhibiti na imeiagiza kutafuta Mkaguzi wa Ndani mara moja na hatimae ikamilishe kasoro zilizoorodheshwa na Mdhibiti.

Hoja Nam 39.2 kuhusu Wadaiwa wa Hoteli ya Bwawani Tshs 21,779,600 na USD 1369.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kuwa juhudi za kuwadai wadaiwa hao zinaendelea.

MAONI YA KAMATI:
Uongozi wa Hoteli uchukue hatua za haraka kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa.

5.0 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO.

5.1 SAUTI YA TANZANIA ZANZIBAR.

Hoja nam. 42.1 Kuhusu Taarifa za madeni. Sauti ya Tanzania Zanzibar ina wadaiwa wa jumla ya Tsh. 19,547,000/ kwa Taasisi za Serikali na Taasisi binafsi.

MAPITIO YA KAMATI:
Sauti ya Tanzania Zanzibar imechukua juhudi mbali mbali katika kudai madeni hayo, ikiwa ni pamoja na kuzungumza na viongozi wa Taasisi hizo na hatimae kufanikiwa kulipwa Tsh. 1,482,000 na hivyo deni hilo limebakia Tsh. 18,065,000/-.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaitaka Sauti ya Tanzania Zanzibar iendelee kudai madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuchukua hatua za kisheria kwa wadaiwa.

6.0 WIZARA YA KAZI, VIJANA, MAENDELEO YA WANAWAKE NA WATOTO.

Hoja nam. 41.1 Kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu za mwisho wa mwaka.

Kukosekana kwa idadi halisi ya fedha taslim za Wahisani wa Maendeleo.

Ukaguzi umeshindwa kupata idadi halisi ya fedha taslim, vifaa au nyenzo za kufanyia kazi za maendeleo kutoka kwa wahisani kwa vile hazikuoneshwa katika hesabu za mwisho wa mwaka za Wizara.

MAPITIO YA KAMATI:
Wakati kamati ilipofika kwa ukaguzi hesabu hizo zilionyeshwa zikiwa na fesa taslim za Wahisani wa maendeleo, ambapo Mchango wa Serikali ni Tsh. 27,900,000 na Mchango wa Wahisani ni Tsh. 145,755,800 ambazo jumla ni Tsh. 173,653,800.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inashauri kuzingatiwa kwa majibu ya Wizara ili hoja hii isijirejee tena.

6.1 IDARA YA MFUKO WA KUJITEGEMEA:

Hoja nam. 40.1 Kuhusu Marejesho ya Mikopo ya Mfuko kupitia 'Account' No. 021103000512.

MAPITIO YA KAMATI:
Ni Kweli kwamba mikopo hiyo yenye thamani ya Tsh. 15,256,500/- imetolewa kwa wananchi mbali mbali wa mikoa yote ya Unguja. Katika kufuatilia mikopo hiyo, Idara imewaandikia barua za wito kwa lengo la kuwasisitiza kulipa kupitia redioni, kupita nyumba hadi nyumba, kuwapigia simu, kupeleka barua kwa wadhamini wao na kuwapatia taarifa Masheha wao. Hata hivyo, baada ya juhudi hizo, deni hilo ambalo halijalipwa hadi Kamati ilipopita kwa ukaguzi ni Tsh. 10,846,500/-.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kuzingatia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inakusudia kupata muda wa ziada kuwaita wadaiwa wote na kuzungumza nao ili kutafuta namna ya kulitatua tatizo hili. Hata hivyo, Kamati inaigiza Idara kufuatilia suala hili kisheria.

7.0 WIZARA YA MAJI, UJENZI, NISHATI NA ARDHI.

7.1 IDARA YA ARDHI NA USAJILI:

Hoja nam. 34.1 Kuhusu kukosekana kwa ukaguzi kuhusiana na fedha Tsh. 360,593,412/40 zilizotolewa kutoka hesabu ya mapato (revenue) kwenda kwenye hesabu nyingine nambari 021101000091.

MAPITIO YA KAMATI:
Hoja hiyo ni sahihi kutokana na Wizara kupokea agizo kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi kutokana na "Standing Order" iliyowasilishwa Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ) na kutumwa nakla kwa Wizara kupitia barua MFEA/M.30/412/161, kwa lengo la kuimarisha ukusanyaji wa mapato ya Serikali yanayotokana na Mawizara.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imelifutilia suala hili hadi Wizara ya Fedha na Uchumi na kufanikiwa kupata usahihi wa risiti ya mapokezi ya fedha hizo. Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi toleo la 2009, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 34.2 Kuhusu madeni ya kodi ya Ardhi ya US $ 1,554,091.80

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kuwa madeni hayo yamepelekwa Bodi ya Mapato ya Zanzibar (ZRB) kwa lengo la kufuatiliwa wadaiwa hao kwa karibu zaidi na kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa haraka.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inakubaliana na hatua hiyo na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (b) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005 Kamati inaomba ipatiwe taarifa ya maendeleo ya ukusanyaji wa madeni hayo kutoka Wizara ya Maji, Ujenzi, Nishati na Ardhi ili ifahamu maendeleo yaliyofikiwa katika suala hilo.

Madeni ya kodi za nyumba, Tsh. 134,945,938/-

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba deni hilo ni Tsh. 175,800,145/- na sio 134,945,938/-. Wizara kupitia Idara ya Nyumba bado inaendelea kudai madeni hayo ikiwa ni pamoja na kufikisha Mahakamani jumla ya kesi 60 na kutolewa uamuzi. Aidha Wizara imeunda Tume ya kuwatambua wale wote wanaodai kupewa nyumba hizo na Marehemu Mzee Abeid Amani Karume.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishwa na maelezo ya Wizara na hivyo inahitaji kukutana na Mhe. Waziri na Naibu Waziri kupata ufafanuzi wa suala hili hadi tunaadika ripoti hii suala hilo halikuweza kufanyika.

8.0 WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA:

Hoja nam 32.1 Kuhusu Vifaa ambavyo havikuingizwa kwenya Daftari la Ghalani (Store Ledger) Tsh. 9,577,580.00

MAPITIO YA KAMATI:
Vifaa vilivyokuwa kavikuingizwa katika Daftari la Ghalani wakati wa ukaguzi, wakati Kamati ilipokuwa ikifanya ukaguzi ilivikuta vifaa hivyo vimeshaingizwa katika Daftari la Ghalani.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 33.1

- **Uvamizi wa Mashamba:**

Ukaguzi ulibaini kuvamiwa kwa mashamba mbali mbali yanayomilikiwa na Wizara.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati ilitembelea maeneo ya Kijichi, Kituo cha Utafiti, Kizimbani na Selemu na kushuhudia uvamizi huo, kwa mfano shamba la Kijichi lililokuwa na Hekta 150, Hekta 100 zimeshavamiwa na Hekta 50 tu zimebaki na Hekta 66 zimevamiwa katika Hekta 240 katika shamba la Kizimbani, na hekta 67,000 za shamba la Makurunge zimevamiwa na zimebakia hekta 6217. Kamati haikuelezwa hatua yeyote iliochukuliwa ya kuzuia uvamizi huo ikiwa ni pamoja na kutokuwa na hati miliki ya mashamba hayo.

MAONI YA KAMATI.
Kamati imeagiza Wizara ya Kilimo kupatiwa ramani halisi za mashamba hayo pamoja na Hati za miliki.

Kuhusiana na Mashamba yaliyopo Tunguu, Mpiga Duri, Maruhubi Kituo cha kuegesha mifugo na Mtoni Karakana, Kamati haijapata muda wa kutosha wa kufuatilia kazi hiyo na inatarajia itafanyika katika kipindi kijacho cha kazi za Kamati.

- **Vifaa ambavyo havikuonekana kwa ukaguzi:**

MAPITIO YA KAMATI:

Kamati ilifahamishwa kwamba, Trackta SMZ 5488 lipo na vifaa vilivyobakia vipo katika Shamba la Kilombero vikiwa vichakavu sana.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inahitaji muda wa kwenda kuviona vifaa hivyo.

- **Mali ambazo hazikuingizwa katika Hesabu za mwisho wa mwaka:**

MAPITIO YA KAMATI:
Wizara imekiri kwamba haikuingiza mali hizo katika Hesabu za mwisho wa mwaka na hivi sasa tayari imesharekebisha kasoro hizo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inahitaji uthibitisho kwamba kweli mali hizo zimeshaingizwa katika Hesabu za Mwisho wa Mwaka ili iweze kupata uhakika wa marekebisho yaliyofanywa.

8.1 KARAKANA YA MATREKTA:
Hoja nam. 32.2 Kuhusu madeni ya muda mrefu wanayodaiwa wateja mbali mbali yenye thamani ya Tsh. 112,446,904/20.

MAPITIO YA KAMATI:
Kweli madeni hayo yanadaiwa kwa muda mrefu sasa bila ya mafanikio ya kulipwa. Aidha, Karakana ilichukua juhudi za kudai kwa utaratibu wa kuwaandikia barua wadaiwa mbali mbali bila ya mafanikio.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kuwa deni hilo kwa asilimia 90% wanadaiwa Wizara ya Kilimo hivyo Wizara italilipa deni hilo kwa kuwanunulia vifaa vya kutendea kazi katika Karakana ya Matrekta.

8.2 IDARA YA UVUVI NA MAZAO YA BAHARINI:
Hoja nam. 55.1 kuhusu Utelekezaji wa Miradi Kifedha:

- **MRADI WA WA MPANGO WA KUENDELEZA HUDUMA ZA KILIMO (ASSP).**

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 mpango wa kuimarisha huduma za kilimo uliidhinishiwa kutumia jumla ya Tsh. 2,432,616,000/- lakini hadi kufikia June 2008, iliweza kuomba na kutumia Tsh. 1,466,007.260.78 hali hii inaonesha kuwa kuna upungufu wa jumla ya Tsh. 966,608,739.22 ambazo hazikuombwa na hazikutumika.

- **MRADI WA KUENDELEZA HUDUMA ZA SEKTA YA KILIMO SEHEMU YA UFUGAJI (ASDP-L)**

Ukaguzi ulibaini kuwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 mpango wa kuendeleza huduma sekta ya Kilimo sehemu ya Ufugaji uliidhinishiwa kutumia jumla ya Tsh.1,697,912,000/- kati ya hizo Tsh. 897,910,000/- ni msaada wa utaalamu na Tsh. 999,254,000/- kwa kazi za kawaida, lakini hadi kufikia Juni 2008 iliweza kuomba na kutumia Tsh. 432,280,061.58 hali hii inaonyesha kuwa kuna upungufu wa jumla ya Tsh.556,973,938.42 ambazo hazikuombwa na hazikutumika.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati ilifahamishwa kuwa, wakati wa ukaguzi, Miradi hiyo ilikuwa ipo katika hatua za mwanzo za utekelezaji, hivyo, taarifa zake hazikuwea kupatikana kwa ukamilifu.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inahitaji kuifanyia kazi tena hoja hii.

Hoja nam. 56.0 Unahusu Utekelezaji wa Mradi Kifedha. Mradi wa Kuhifadhi Mazingira ya Baharini na Ukanda wa Pwani (MACEMP).
Ukaguzi umebaini kuwa katika mwaka wa fedha 2007/2008 Mradi ulipokea USD 262,123.03 kwa mwaka husika kutoka Mfuko wa GEF kati ya fedha zilizoidhinishwa USD 1,056,875 kwa mwaka husika. Hali hii inaonesha kuwa kuna upungufu wa USD 794, 751.97 ambazo hazikutolewa.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kuwa hali hiyo inatokana na mfumo na utaratibu mzima wa manunuzi wa Benk ya Dunia ambapo utaratibu huo unachukua muda mrefu kabla ya Taasisi kuweza kufanya manunuzi husika.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeagiza kupatiwa Ripoti za Miradi ili kuelewa uendeshaji wa Miradi hiyo.

Hoja nam. 56.2 Vifaa ambavyo havikuingizwa katika Daftari la Ghalani vyenye thamani ya Tsh. 36,400,000 na USD 58,100.

MAPITIO YA KAMATI:
Vifaa vilivyokuwa havikuingizwa katika Daftari la Ghalani wakati wa ukaguzi, baaada ya Kamati kuvifuatilia vifaa hivyo katika sehemu mbali mbali vilimoekwa, vilionekana na kukutwa tayari vimeshaingizwa katika Daftari la Ghalani.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inasisitiza kufuatwa Sheria na taratibu za manunuzi na matumizi ya vifaa.

9.0 WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII.

Hoja nam 28.1 kuhusu malipo yasiyo na stakabadhi ya Tsh. 1,469,000/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi ziliwasilishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kuzingatia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja nam 28.2 kuhusu malipo yasiyokuwa na vielelezo (Supporting Documents) Tsh. 5,000,000/-

MAPITIO YA KAMATI:
Wakati wa ukaguzi wa Kamati, vielelezo hivyo pia havikuweza kupatikana.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inahitaji kupatiwa vielelezo hivyo ili kuthibitisha uhalali wa matumizi hayo.

Hoja nam. 28.3 kuhusu Malipo yasiyo na stakabadhi (Risiti) ya Tsh. 61,379,500/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Baadhi ya vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi vilipatikana. Hata hivyo, hati namba 3/10/2007 yenye hundi namba 086320 ya thamani ya Tsh 31,954,000/- na hati namba 5/11/2007 yenye hundi namba 086345 ya thamani ya Tsh. 23,221,000/- hazikupatikana wakati wa ukaguzi wa Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikufurahishwa na majibu ya Wizara na imeiagiza Wizara kuhakikisha stakabadhi hizo zinapatikana mara moja.

Hoja nam. 28.4 kuhusu Malipo yasiyokuwa na Stakabadhi (Risiti) ya Tsh. 7,269,225.85/-

MAPITIO YA KAMATI:
Stakabadhi zilivyokosekana wakati wa ukaguzi ziliwasilishwa mbele ya Kamati zikiwa zimekamilika.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 28.5 kuhusu Malipo yasiyokuwa na stakabadhi Tsh. 1,245,700/-

MAPITIO YA KAMATI:
Wizara imeweza kuwasilisha hati namba 2/12/2007 yenye hundi namba 640849 ya thamani ya Tsh.233,200/- na imeshindwa kuwasilisha hati namba 8/6/2008 yenye hundi namba T.O ya thamani ya Tsh. 1,012,500/- ili kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haifurahishwi na mwenendo wa Wizara hii ambayo mara nyingi haitilii maanani taratibu za matumizi ya fedha kama zinavyoelekezwa na Sheria. Hivyo, Kamati imeiagiza Wizara kuhakikisha vielelezo vyote vilivyokosekana wakati wa ukaguzi wa Kamati vinapatikana.

10.0 WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA:

Hoja nam. 14.1 Ukaguzi umeshindwa kupata Mkataba wa ujenzi (Ukarabati) wa Afisi ya Hakimiliki, Pemba, invoice na Risiti za manunuzi ya samani hizo, hali iliyopelekea kushindwa kuthibitisha uhalali wa matumizi husika.

MAPITIO YA KAMATI:
Mkataba, Invoice na Risiti za manunuzi zilizokosekana wakati wa ukaguzi, ziliwasilishwa mbele ya Kamati. Hata hivyo, Kamati haikuridhishwa na Mkataba huo wenye mapungufu kadhaa ikiwemo kukosekana muhuri na saini za Wizara na Mkandarasi katika baadhi ya kurasa za makataba huo.Aidha manunuzi ya samani husika hayakufuata utaratibu wa Zabuni.

MAONI YA KAMATI:
Wizara imekiri makosa yaliyojitokeza na kueleza yamesababishwa na elimu ndogo ya maunuzi. Kamati imeitaka Wizara wazirekebishe haraka kasoro zilizojitokeza.

10.1 AFISI YA MRAJIS MKUU WA SERIKALI:

Hoja nam. 15.1 Kuhusu Baadhi ya Mashekhe wanashindwa kurudisha fedha za vyeti vya ndoa na talaka, vyenye thamani ya Tsh. 2,750,000/-

MAPITIO YA KAMATI:
Afisi imekiri kasoro hii na kuieleza Kamati kwamba imefanya juhudi za kuwapelekea Taarifa Mashekhe kuwataka warejeshe fedha hizo ikiwa ni pamoja na kuandaa Semina kwa Mashekhe. Hata hivyo, ni Mshekhe 9 tu wamerejesha feha hizo kati ya Mashekhe 22 walioorodheshwa katika Ripoti ya Mdhibiti.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeitaka Afisi ya Mrajis kuhakikisha kuwa madeni hayo yanalipwa.

Ukusanyaji wa Mapato:
Ukaguzi umebaini Afisi ya Mrajis inajikopesha fedha za mapato zinazokusanywa katika Afisi hiyo huku urejeshwaji wake unatia mashaka ambapo jumla ya Tsh. 1,645,600/- hazijarejeshwa.

MAPITIO YA KAMATI:
Hoja ya Mdhibiti inathibitisha hadi wakati wa Kamati ilipokuwa katika Afisi hiyo kwa ukaguzi fedha hizo bado hazijarejeshwa .

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishwa na tabia ya kujikopesha ambayo ni kinyume na Sheria na Kanuni za Fedha. Aidha inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa kuisaidia ama kueka utaratibu wa Afisi kuwa na Fedha za ziada zitakazotumika kwa matumizi ya dharura.

Wizi wa Kompyuta 4.
Ukaguzi umegundua kompyuta 4 zimeibiwa katika hali ya kutatanisha na wala Afisi ya Mrajis haikuchukua hatua zozote kuhusiana na wizi huo.

MAPITIO YA KAMATI:
Afisi imekiri kutokea kwa wizi huo ulitokea bila ya kuvunjwa kwa milango ya Afisi hiyo na uliofanyika katika vipindi viwili tofauti; kipindi cha kwanza kuliibiwa komputa moja na baadae zikaibiwa nyengine tatu. Kamati imeelezwa kuwa Afisi imechukua jitihada za kuiarifu Polisi juu ya tukio hilo kwa barua nambari IMS/JFV/3/Vol.III ya tarehe 24/06/2008 iliyopelekwa kwa Mkuu wa Kituo cha Polisi, Malindi.

MAONI YA KAMATI:
Pamoja na majibu hayo, Kamati haikuridhishwa na jitihada zilizochukuliwa na Afisi ya Mrajis katika kupambana na wizi huo kwani tokea tarehe 24/06/2008 iliporipotiwa wizi huo katika kituo cha Polisi Malindi hakuna hatua nyengene yeyote iliyochukuliwa ya kukabiliana na wizi huo. Kamati inahitaji kulifanyia kazi zaidi suala hili.

11.0 AFISI YA WAZIRI KIONGOZI.

11.1 TUME YA UKIMWI, ZANZIBAR.

Malipo yasiyokuwa na Vielelezo (supporting Documents) jumla ya Tsh. 5,918,500/-

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi, viliwasilishwa mbele ya Kamati na kufahamishwa kwamba, vilikosekana kwa sababu vilikuwa chini ya ukaguzi wa nje (external Auditors).

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeridhishwa na majibu hayo, na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

12.0 WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI:

Hoja nam 27.1 kuhusu Kukosekana kwa nyaraka za uingizaji wa fedha zenye thamani ya Tsh. 6,098,341,983/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Nyaraka zilizokosekana wakati wa ukaguzi, ziliwasilshwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeridhishwa na majibu hayo, na kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

12.1 IDARA YA NYARAKA, MAKUMBUSHO NA MAMBO YA KALE:

Hoja nam. 24.2 Kuhusu ucheleweshaji wa upelekaji wa mapato Bank.

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli kasoro hizo zipo kutokana na Idara kujikopesha fedha hizo kutokana na uhaba wa fedha za kukimu matumizi ya dharura.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikukubalina na tabia hiyo na kuitaka Idara kujirekebisha mara moja. Hata hivyo, Kamati inaishauri Serikali kuangalia uwezekano wa Idara kuhakikisha inakua na fedha za kukimu matumizi ya dharura.

Hoja nam. 24.3 kuhusu Idara imeshindwa kutekeleza malengo ya Mradi hali ya kuwa fedha za Mradi ziliingizwa sawa na asilimia 15.7 ya makadirio.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kuwa wakati wa ukaguzi, fedha hizo za Mradi zilikuwa bado hazijaingizwa na kuweza kutumika kwa wakati. Hata hivyo, fedha hizo tayari zimeshatumika kwa mujibu wa malengo yaliyokubaliwa.

M**AONI YA KAMATI:**
Kamati imeridhishwa na majibu ya Idara baada ya kuthibitisha uhalali wa matumizi ya fedha hizo.

12.2 SHIRIKA LA HUDUMA ZA MAKTABA:

Hoja Nam 25.2 kuhusu hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi zenye thamani ya Tshs 7,898,360-/

MAPITIO YA KAMATI
Ukaguzi ulibani kuwa hati zote arobaini (40) za malipo zilizokosekana wakati wa ukaguzi zilipatikana wakati wa ukaguzi wa Kamati. Kamati ilelezwa kuwa wakati wa ukaguzi hati hizo hazikupatika kwa vile muhasibu alikuwa hayupo.

MAONI YA KAMATI
Kamati haikufurahishwa na kitendo cha kutotunzwa kumbukumbu muhimu vizuri na ilitoa onyo kutorudia tena suala hilo.

Hoja Nam 25.3 kuhusu upotevu wa fedha jumla ya Tshs 26,963,500=/

MAPITIO YA KAMATI
Ukaguzi umebaini kuwa kuna malipo yamefanyika kwa njia zisizo sahihi kwani matumizi hayo yamefanyika bila ya kuwepo kumbukumbu na vitabu vya kuwekea kumbukumbu za hesabu. Kamati imeelezwa kuwa upotevu huo umesababishwa na mhasibu aliyekuwepo wakati huo na kwa hivi sasa ametoroka na hayupo nchini suala hili limeripotiwa Polisi na hatua za kumtafuta zinaendelea.

MAONI YA KAMATI
Kwa kuwa suala hili limesharipotiwa Polisi, Kamati inasuburi maelezo zaidi kutoka Shirika la Maktaba.

12.2.3 CHUO KIKUU CHA TAIFA SUZA.
Hona nam. 26.1 kuhusu Malipo yasiyo na Stakabadhi ya Tsh. 6,718,975/-

MAPITIO YA KAMATI:
Stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi wa Mdhibiti, ziliweza kuwasilishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005 Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

UFAFANUZI WA HOJA ZA MKAGUZI NA MDHIBITI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI, KWA TAASISI ZA PEMBA:

13.0 WIZARA YA UTALII, BIASHARA NA UWEKEZAJI.
13.1 KAMISHENI YA UTALII:

Hoja Nam. 57.10 kuhusu kutokuwasilishwa fedha za mapato ZRB- Pemba, USD 12,775. Kamisheni inakusanya mapato katika hesabu namba 042108000001 ya fedha za kigeni katika Benki ya Watu wa Zanzibar kinyume na utaratibu wa kuzihaulisha fedha hizi kwenda katika Hesabu ya Bodi ya Mapato (ZRB) Pemba utaratibu huu kwa sasa haufuati na badala yake mapato hayo yanahaulishwa kupelekwa katika akunti ya kamisheni ya utalii Unguja.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamisheni ya Utalii imekiri juu ya kutowasilisha fedha za mapato ZRB Pemba kama sheria inavyoelekeza kutokana na utaratibu waliokuwa wakiutumia ulikuwa ndio uliozoeleka kuziwasilisha fedha hizo katika Afisi za Kamasheni Unguja badala ya kuziwasilisha Bodi ya Mapato Pemba. Hata hivyo, baada ya kupata maelekezo ya Mdhibiti na kufahamu muongozo sahihi wa kisheria, Kamisheni imesharekebisha suala hilo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imesisitiza kufuatwa utaratibu wa sheria za fedha unavyotaka na si vyenginevyo.

14.0 WIZARA YA KILIMO, MIFUGO NA MAZINGIRA:

Hoja Namba 57.11 **Kuhusu Vifaa vilivyonunuliwa ambavyo havikuingizwa kwenye daftari la vifaa vyenye thamani ya Tsh. 1,720,000/-.**

MAPITIO YA KAMATI:
Wizara imekiri kwamba vifaa hivyo havikuingizwa wakati wa ukaguzi. Hata hivyo, wakati Kamati ilipokutana na Wizara, vifaa hivyo tayari vilikwisha ingizwa katika daftari la vifaa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeagiza daftari hilo lipelekwe kwa Mdhibiti ili alikague na hatimae Kamati ijuilishwe.

15.0 WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

Hoja Nam. 57.5 Kuhusu upotevu wa Mishahara Tsh. 4,878,256/-. Kwamba baada ya ukaguzi, imebainika kwamba kuna upotevu wa mishahara ya wafanyakazi 48 yenye jumla ya Tsh. 4,878,256/- katika kitengo cha Micheweni Cottage kwa mwezi wa March 2008.

MAPITIO YA KAMATI:
Wizara imekiri kutokea kwa upotevu huo, hadi tunaandika ripoti hii wafanyakazi 25 hawajalipwa mishahara yao. Wizara iliziitaarifu taasisi husika na hatimae watuhumiwa walipelekwa Mahakamani kupitia kesi ya Jinai, Namba 33 ya 2008 ambapo kutokana na kutokupatikana kwa taarifa muhimu zinazowaunganisha washtakiwa na kosa lao, Upande wa Kuendesha Mashtaka uliamua kuliondosha Mahkamani shauri hilo, na hatimae washtakiwa kuachiwa huru na Mahkama tarehe 06/08/2008. Upotevu huu ulisababishwa na kutokuwepo kwa Tajuri la kuhifadhia fedha, kinyume na kifungu cha 140 cha Kanuni za Fedha, 2005 na walinzi kituoni hapo walikuwa wachache. Kamati imeelezwa kuwa tajuri hilo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imelichukulia suala hili kama ni uzembe uliofanyika na kusababisha kuibiwa kwa mishahara,aidha Kamati imesisitiza kuharakisha kuwalipa wafanyakazi 25 mishahara yao ambapo hadi wakati Kamati ilipokuwa ikifanya ukaguzi mishahara hiyo ilikuwa bado hawajalipwa.

MADENI MBALI MBALI AMBAYO WIZARA YA AFYA INADAIWA.
Ukaguzi uligundua madeni mbali mbali ya muda mrefu ambayo Wizara inadaiwa na wafanya biashara, Taasisi za Serikali na baadhi ya Watumishi wake wa Wizara ya Afya yanayofikia jumla ya Tsh. 144,448,351/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Madeni hayo yalikuwa 164,612,006/- Wizara ya Afya na Ustawi jamii kwa mashirikiano na Wizara ya Fedha na Uchumi, ilifanya uhakiki wa madeni na hatimae April 2008 wafanya biashara 20 walilipwa na kubakia 144,448,351/- kama ilivyoripotiwa na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, ambapo Kamati ilielezwa kuwa deni hilo wamekabidhiwa Wizara ya Fedha na Uchumi kwa ajili ya malipo.

MAONI YA KAMATI:
Kutokana na maelezo yaliyotolewa na Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwamba hivi sasa ni deni la Wizara ya Fedha na Uchumi, Kamati imeiagiza Wizara ya Afya kukumbushia malipo ya deni hilo kwa maandishi.

16.0 WIZARA YA NCHI (AR) KATIBA NA UTAWALA BORA:
16.1 MRAJIS WA MAHAKAMA YA MKOA WA KUSINI, PEMBA:

Hoja Nam. 57.13 Inahusu Malipo ya Masurufu (Imprest) ambayo hayana marejesho, jumla ya Tsh. 4,356,000

MAPITIO YA HOJA
Ukaguzi umebaini kuwa kuna malipo yalitumika kwa ajili ya kuwalipa mshahidi lakini marejesho ya masurufu hayakupatikana kwa ukaguzi.Wakati wa ukaguzi wa Kamati marejesho hayo hayakupatika kwa kuwa muhusika aliyekabidhiwa marejesho hayo alikuwa amehamishiwa kazi Unguja Kamati baada ya kufuatilia hoja hii Unguja ilikuta vielelezo vyote vya marejesho hayo vipo na vimekamilika.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishwa na utaratibu huu wa kuotofunganisha kwa pamoja marejesho ya masurufu na vielelezo vyake na inasisitiza kutorudiwa tena suala hilo.

17.0 WIZARA YA MAJI, UJENZI, NISHATI NA ARDHI.

Hoja Nam. 57.2 Kuhusu madeni mbali mbali ambayo Wizara inadai kwa watu binafsi na taasisi za Serikali yenye thamani ya Tsh. 36,951,580/- na Fedha za kigeni USD $ 67,775/-

MAPITIO YA KAMATI:
Kuhusiana na madeni ya fedha za kigezi, USD $ 67,775/- Kamati haikupata majibu ya kuridhisha na hivyo, Wizara itafanya utaratibu wa kuijibu Kamati. Aidha madeni mengine ambayo hayajalipwa hatua za kuwapeleka wahusika mahakamani zitachukuliwa.

MAONI YA KAMATI:
Hadi tunaandika Ripoti hii bado hatujapata maelezo yoyote kuhusu suala hili.

17.1 MAMLAKA YA MAJI:

Hoja Nam. 57.4 Kuhusiana na Madeni 4,503,000/- yanayodaiwa kwa Taasisi za Serikali na za watu binafsi.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imeelezwa kuwa kati ya 4,068,000/= zinazodaiwa kwa Taasisi na Watu binafsi ni Tshs 10,000/- tu ndizo zilizolipwa hadi tunaandika ripoti hii, wakati Taasisi za Serikali hazijalipa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeiagiza Mamlaka kuwakatia huduma ya maji wadaiwa wa Taasisi binafsi ili iwe kama ni adhabu kwa wenye madeni. Iwapo Taasisi yoyote itakwenda kinyume kwa kujiungia maji bila ya idhini ya Mamlaka, hatua za kuwapeleka Mahakamani zinaweza kuchukuliwa. Kwa upande wa Taasisi za Serikali, Mamlaka ishirikiane na Wizara ya Fedha na Uchumi kuhakikisha madeni hayo yanalipwa.

18:0 WIZARA YA MAWASILIANO NA UCHUKUZI:PEMBA

Hoja Nam. 57.1 Kuhusu Vifaa chakavu. Kwamba, Wizara imeviacha vifaa chakavu vilivyonunuliwa kwa thamani kubwa na havifanyi kazi tena. Afisi ya Mdhibiti imeshauri kuandaliwa utaratibu mzuri wa kuuzwa kwa vifaa hivi ili Serikali kupata mapato.

MAPITIO YA KAMATI:
Katika kutekeleza ushauri huo wa Afisi ya Mdhibiti, Wizara imeuza gari mbili chakavu ambazo ni Crane Truck Mercedes Benz SMZ 3446 na Dump Truck Mercedes Benz SMZ 4496. Aidha, Wizara imelazimika kusitisha zoezi hilo la kuuza kutokana na agizo la kusitisha uuzaji wa mali za Serikali lililotolewa na Wizara ya Fedha tarehe 25 Novemba, 2009 kwa barua yenye kumbu kumbu MFEA/PS/M.30/4/05/69 na barua ya Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi ya tarehe 1/12/2009 yenye kumbu kumbu MOCT/F.10/C.1/VOL II/79.

Kutokana na hali hii, kuna vifaa vinavyofanyiwa matengenezo ikiwa ni pamoja na Bulldozer Komatsu, SMZ 4567, Dump Truck, Hino SMZ 5141 na Dump Truck, Jie Fang SMZ 5940. Viko vilivyofanyiwa matengenezo na kufanya kazi ambavyo ni Roller A/Buford SMZ 2409, Fuel Bowzer, Leyland SMZ 2500, Dump Truck, Hino SMZ 5134 na SMZ 5137 na Dump Truck Jie fang SMZ 5938, Excavator Caterpillar. Aidha vifaa ambavyo vimo katika orodha ya kuuzwa ni Roller SMZ 2308, Dump Truck Isuzu, SMZ 5695, SMZ 5696, SMZ 5697, SMZ 5698, Dump Truck Jie fang SMZ 5937, SMZ 5939 na Skip handler M/Benz SMZ 4497. Roller A/Buford SMZ 2306, Roller Bomag na Paver Blawknox SMZ 4565 vimewekwa spare, huku Engine ya Tractor Deutzfahr SMZ 3402 imepelekwa Unguja.

MAONI YA KAMATI:

Pamoja na hatua za kuuzwa kwa magari hayo mawili, Wizara haikufuata utaratibu wa sheria za uuzaji wa mali za Serikali, ikiwa ni pamoja kutoitisha Tenda. Kamati imeitaka Wizara kufuata utaratibu wa sheria katika uuzaji wa mali za Serikali. Aidha, Kamati inatarajia kwamba baada ya kusita kwa amri hiyo ya uuzaji wa mali za Serikali, Wizara itaendelea kutekeleza ushauri wa kuuza vifaa hivyo chakavu kwa kufuata utaratibu wa kisheria.

18.1 SHIRIKA LA BANDARI:PEMBA

Hoja Nam. 57.3

Kuhusu Madeni yanayodaiwa na Shirika la Bandari, jumla ya Tsh. 17,780,332.40. Ambapo Kampuni ya Hammy Distribution kwa kipindi cha July 2007- June 2008 inadaiwa Tsh. 10,548,321.15; Oryx Oil Company inadaiwa Tsh. 5,187,602.25 na Gapco Oil Company 2,044,409/-.

MAPITIO YA KAMATI:

Shirika limechukua juhudi na kufanikiwa kulipwa na Oryx Oil Company kwa Cheque No. 009672 na 006630 kwa risiti namba 1145 na 1164 za tarehe 20/8/2009 na 14/12/2009. Aidha Gapco Oil Company imelipa deni kupitia Cheque No. 431919 kwa risiti No. 1147 ya tarehe 3/09/2009 Hammy Distribution imelipa Tsh.2,000,000 kupitia Cheque No. 000154 na 000157 kwa risiti namba 1152 na 1161 za tarehe 2/10/2009 na 20/11/2009 na imebaki ikidaiwa 8,548,321.15.

MAONI YA KAMATI:

Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa na Shirika na kulitaka kuendelea kuwadai Hammy Distribution kwa kuweka Mkataba wa namna ya ulipaji wa deni hilo na hatimae Kamati ijuilishwe.

19.0 WIZARA YA HABARI, UTAMADUNI NA MICHEZO: PEMBA

Hoja nam. 57.12 Kuhusu Malipo ya Masurufu (Imprest) ya Tsh. 1,105,000/- yaliyolipwa kupitia vocha mbali mbali zikiwa ni matumizi ya Wizara ambazo hazikupatikana kwa ukaguzi.

MAPITIO YA KAMATI:

Wakati wa ukaguzi kumbukumbu za marejesho ya masurufu hayo hazikupatikana, wakati Kamati ilipofika Wizarani, kumbu kumbu hizo zilipatikana.

MAONI YA KAMATI:

Kamati inashauri kufutwa kwa hoja hii kwa kuzingatia kifungu cha 51 (5) (c) ya kanuni ya fedha, 2005.

20.0 WIZARA YA NCHI (AR) TAWALA ZA MIKOA NA VIKOSI VYA S.M.Z

20.1 AFISI YA MKUU WA MKOA WA KASKAZINI (PEMBA):

Hoja nam. 57.6 Kuhusu Ununuzi wa Samani kwa Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani-Pemba zenye samani ya Tsh. 71,620,000/-

MAPITIO YA KAMATI

Ukaguzi umebaini kuwa kuna mkataba uliofungwa baina ya Afisi ya Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Pemba na Ushirika wa AL-Sahil Consruction Co-operative Society kwa ajili ya ununuzi wa samani (farnitures) za Wilaya ndogo Kojani Mkataba huu ulifungwa 1/7/2007.Yafuatayo yalijitokeza katika utekelezaji wa mkataba huu:

- Upungufu wa samani zenye thamani ya Tshs 21,380,000/- ambazo tayari zimeshalipwa kwa mujibu wa Mkataba lakini hazikuonekana katika Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani.
- Ushirika wa AL SAHAL CONSTRUCTION CO-OPERATIVE SOCIETY umepokea ziada ya Tshs 3,380,000/- kinyume na mkataba husika kwani thamani ya mkataba ni Tshs 71,620,000/-lakini fedha alizolipwa Mkandari huyo ni Tshs 75,000.000/-

Kuhusu malipo ya ziada ya Tshs 3.380,000/- Kamati imeelezwa kuwa Mkandarasi alilipwa fedha za fanicha pamoja na fedha za ujenzi wa ukuta.

Katika ufuatiliaji wa hoja hii kwenye Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani, Kamati iliiagiza tena Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kewnda Kojani kufanya ukaguzi tena. Kutokana na barua iliyotoka Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu, Pemba ya tarehe 24/2/2010 yenye kumbukumbu namba PBW.2, ukaguzi huo ulibaini kuwa samani (furnitures) zilizokosekana wakati wa ukaguzi wa awali zimeonekana. Pamoja na kuonekana kwa samani hizo, ukaguzi huu ulibaini yafuatayo:-

- Meza nne (4) kubwa za Afisi hiyo zenye thamani ya Tshs, 2,280,000/- hazikuonekana.
- Bei za kununulia samani hizo ni kubwa, hazilingani na samani husika.
- Kiwango (Quality) cha samani zilizopo hazilingani na ile iliyoainishwa na kukubalika katika Mkataba.

MAONI YA KAMATI
Kamati haikuridhishwa na hali hii ya ubadhiriru wa fedha.

20.2 JESHI LA KUJENGA UCHUMI.
Hoja nam. 57.8 Kuhusiana na madeni ambayo J.K.U inadaiwa ya Tsh. 44,267,600/- na inayodai kwa Taasisi mbali mbali, Tsh. 52,364,558/-

MAPITIO YA KAMATI:
Kikosi cha JKU kimeweza kulipa deni la Tshs 5,500,000/ kati ya fedha wanazodaiwa na zimebaki Tsh. 38,7676,00/- ambazo hazijalipwa na kati ya Tsh.52,364,558 wanazozidai kwa Taasisi mbali mbali, Tsh.11,640,770/- zimelipwa na zimebakia 40,723,788/-.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba madeni hayo ni ya mda mrefu na ni mzigo kwa J.K.U kwa kuzingatia ukweli kwamba, J.K.U (P) hawana sub-votes yao na pia wanapata ruzuku ndogo kutoka Serikalini. Kamati inaishauri Serikali kuitizama hali hii na hatimae kuitatua, ili waweze kujiendesha kwa ufanisi.

20.3 BARAZA LA MJI, CHAKE CHAKE:

Hoja nam. 57.7 Kuhusu deni la Baraza la Mji- Chake Chake Tsh. 14,832,000/- linalotokana na ununuzi wa samani (Furnitures) zilizokopwa kutoka duka la City Furniture Dar es Salaam kwa ajili ya Afisi ya Baraza la Mji, Chake Chake.

MAPITIO YA HOJA:
Mpaka Kamati inafanya kazi katika Afisi ya Baraza la Mji, Chake Chake bado haijalipa deni hilo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaagiza deni hilo kulipwa mara moja kama Baraza la Mji, Chake Chake lilivyoahidi.

20.4 HALMASHAURI YA WILAYA YA CHAKE CHAKE:
Hoja nam. 57.9 Kuhusu kutokuwepo Tajuri la kuhifadhia fedha katika chumba cha Mshika Fedha.

MAPITIO YA KAMATI:
Halmashauri imeliona tatizo hilo na kuliwasilisha Wizara ya Fedha na Uchumi, Pemba kwa ajili ya kupatiwa Tajuri hilo.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaiagiza Wizara ya Fedha na Uchumi, kuharakisha upatikanaji wa Tajuri hilo ili liweze kutumika kama inavyokusudiwa.

UKAGUZI KATIKA MASHIRIKA YA SERIKALI

21.0 SHIRIKA LA BIMA

Hoja nam. 47.1 kuhusu Malipo ya Tsh. 19,920,450/- yalifanyika bila ya stakabadhi.

MAPITIO YA KAMATI:
Hati zilizokosekana wakati wa ukaguzi ziliwasilishwa mbele ya Kamati. Kamati pia ilifahamishwa kwamba kwa malipo yaliyohusiana na fidia, Shirika imelazimika kuyafanya bila ya risiti.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeelekeza kwamba, hoja ya kutotolewa kwa risiti katika malipo ya fidia, ilipaswa kuelezwa kwa Wakaguzi na wao ndio wangeifanyia maamuzi. Hata hivyo, Kamati imeipokea taarifa hii.

Hoja nam. 47.2 Kuhusu vifaa vyenye thamani ya Tsh. 4,077,100 ambavyo havikuingizwa katika Daftari la ghalani (Store Ledger).

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli wakati wa ukaguzi vifaa hivyo vilikuwa bado havijaingizwa katika Daftari la Ghalani. Hata hivyo, wakati wa kazi za Kamati, ilishuhudiwa vifaa hivyo tayari vimeshaingizwa katika Daftari la Ghalani.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeipokea taarifa hii na kuthibitishwa kuingizwa katika Daftari hilo.

Hoja nam. 47.3 Kuhusu Malipo ya Tsh. 34,848,541.81 yaliyofanyika bila ya Stakabadhi.

MAPITIO YA KAMATI:
Stakabadhi zilizokosekana wakati wa ukaguzi, tayari kwa ukamilifu wake zimepatikana na kuwasilishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inashauri kwa kuzingatia kifungu cha 151 (5) (c) cha Kanuni za Fedha, 2005 hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 47.4 Kuhusu baadhi ya Mawakala kukaa na fedha nyingi bila ya kuziwasilisha Bank kwa wakati.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imefahamishwa kwamba, kwa mujibu wa Kanuni ya Bima ya mwaka 1998, inaruhusu madalali kukaa na fedha wanazozikusanya si zaidi ya siku 60 na hivyo, Madalali wote walikaa na fedha hizo ndani ya muda uliowekwa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishwa na majibu haya na inaamini yangepaswa kujibiwa mbele ya Maofisa wa Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu. Aidha, Kamati inasisitiza fedha zisicheleweshwe kupelekwa Benki kama Sheria inavyoelekeza.

22.0 SHIRIKA LA BANDARI:

Hoja Nam. 48.1
Matokeo baada ya Kufunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka.
Kuhusu Uwezo wa Shirika kujiendesha kwa faida: Takwimu zinaoesha wazi kwamba, Shirika linapata faida lakini faida hiyo inaendelea kupungua mwaka hadi mwaka. Afisi ya Mdhibiti ilishauri Shirika lipunguze gharama za kiutendaji, aidha liwe makini katika kufuatilia biashara ya fedha za kigeni duniani kwa kuhamisha fedha kutoka aina moja ya fedha kwenda aina nyengine amayo itakuwa na thamani kubwa zaidi kwa wakati husika.

Mapitio na maoni ya Kamati:
Kamati pia imfahamishwa kwamba, ujenzi wa gati ya Malindi ikiambatana na kupanda kwa gharama ya ujenzi kwa upande mwengine pia umechangia kupungua kwa faida ya Shirika.

Kuhusu Shirika kupunguza gharama za kiutendaji, Kamati imefahamishwa ugumu wa kutekeleza agizo hili kutokana na uwezo wa Shirika kulipa mafao ya wastaafu ikiwa pia ni pamoja na malipo ya ZSSF. Hata hivyo, Kamati imelitaka Shirika kutekeleza agizo hili kwa maslahi ya Shirika.

Kuhusu Wadaiwa wa Shirika (Trade Debtors);
Shirika lina kiwango kikubwa cha wadaiwa, ambapo kwa mwaka 2007 ni jumla ya Tsh. 2,417,138,133.64 baada ya kutoa Tsh. 604,284,533.20 ambazo Shirika linadhani hazilipiki (Provision for bad debts). Deni hili ni la muda mrefu na linaathiri sura halisi ya mali za mpito za Shirika. Afisi ya Mdhibiti wa Hesabu ililishauri Shirika kutafuta utaratibu wa Sheria ili kufuta wadaiwa hao na hatimae sura halisi ya mali za mpito ipatikane.

Maoni ya Kamati:
Kamati imeliagiza Shirika kulichukulia hatua za Kisheria suala la madeni ili kuweza kutoa sura halisi ya ya mali za mpito.

Ziara ya Kamati katika Bandari ya Malindi:

Kwa kuzingatia kifungu cha 113(3)(c) cha Kanuni za Baraza la Wawakilishi, toleo la 2009, Kamati ilitembelea Bandari ya Malindi na hatimae kufahamu na kutoa ushauri ufuatao:

Ujenzi wa sehemu ya Abiria, Afisi ya Shirika na Sehemu ya kuegeshea Magari:
Katika juhudi za kuinua uwezo wa Shirika, Shirika linatarajia kufanya ukarabati wa majengo yaliyopo Bandari ya Malindi ili yatumike kama Afisi ndogo ya Shirika, sehemu ya kuhifadhia mafuta, sehemu ya Abiria, sehemu ya kuegeshea magari na kuanzisha kituo cha Taxi. Kukamilika kwa ujenzi huu kutaongeza ukusanyaji wa mapato ya Shirika, ingawaje ujenzi huu mpaka hatua ya kukamilika kwake, utagharimu fedha nyingi ukizingatia kwamba fedha zote zitalazimika kutoka katika Mfuko wa Shirika na uwezo wa Shirika ni mdogo kumudu gharama hizo.

Ukarabati wa Matishali:
Matishali yaliyopo yanahitaji kufanyiwa ukarabati (service) ili yaweze kutumika kwa usalama na ufanisi. Ukarabati huu utaligharimu Shirika takribani 700,000,000/- na utakuwa si chini ya mwezi mmoja. Kamati inaishauri Serikali kulisaidia Shirika.

Uingiaji wa Meli za Kigeni:
Pamoja na kukamilika kwa ujenzi wa Gati ya Malindi, Shirika linakabiliwa na changamoto nyingi sana zikiwemo kuanza ufa wa kudidimia kwa Bandari hiyo, uwezo wa Bandari ni kupokea meli zenye tani isiyozidi 10; uharibifu wa mazingira na zaidi kwa sababu Bandari haina mvungu na hivyo kupelekea hata mazalio ya samaki kutoweka. Kamati inashauri Serikali kulisaidia Shirika kuanzisha Bandari nyengine ya Kisasa maeneo ya Mpiga Duri.

Eneo la matengenezo ya Vyombo, (Chelezoni):
Kamati imefurahishwa na juhudi zinazochukuliwa na Shirika za kutengeneza vyombo vyake na vyombo vya Taasisi nyengine za Serikali na watu binafsi. Hata hivyo, Kamati imesikitishwa na taarifa kwamba, Kikosi cha Kuzuia Magendo (KMKM) kimepeleka chombo chake lakini hakilipi kama inavyotakiwa, imeelezwa kwamba, hivi sasa imefikia jumla ya Tsh. 60,000,000/- zinazodaiwa kwa KMKM.
Kamati inakiagiza Kikosi cha KMKM kulipa deni hilo, ili Shirika lijinasue na hali mbaya ya upungufu wa mapato inayoikabili.

23.0 SHIRIKA LA MELI NA UWAKALA:

Hoja Nam 46.1 kuhusu Matokeo baada ya kufunga Hesabu za mwisho wa mwaka:
Baada ya kufunga hesabu za mwisho wa mwaka, matokeo yafuatayo yamejitokeza:-

Shirika linajindesha kwa hasara kutokana na kushindwa kulipa dhima zake za mpito kwa vile ‘current ratio’ yake ni 0.16:1. Shirika lilishauriwa kuchukua juhudi za kuongeza mtaji wake na kupunguza madeni ili liweze kutoa sura nzuri ya kuendelea kufanya shughuli zake kiufanisi.

Mapitio ya Kamati:
Kamati imefahamishwa ukweli wa uwezo mdogo wa Shirika kulipa dhima zake za mpito na hali hii inatokana na kukithiri kwa madeni. Baadhi ya madeni hayo ni kudaiwa na Benki ya Watu wa Zanzibar (PBZ), Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi na Shirika la Bandari kiasi cha Tsh. 2,137,939,220.09 ambazo ni sawa na asilimia 88.45 % ya wadaiwa wote wa Shirika la Bandari.

Maoni ya Kamati:
Kamati imeshtushwa na hali hii na imeazimia kukutana na Bodi ya Shirika, Mhe. Waziri anaeshughulikia masuala ya Fedha na Uchumi na Mhe. Waziri wa Wizara ya Mawasiliano, ili kuona namna gani ya kulishauri Shirika. Kutokana na muda kuwa mfupi wa kazi za Kamati, Kamati imeshindwa kufanya kikao hicho

Faida inayopata Shirika inapungua mwaka hadi mwaka, na hii inasababishwa na ongezeko la gharama za uendeshaji, uchakavu wa meli za Shirika, pamoja na ongezeko la gharama za kiutawala.

Mapitio ya Kamati:
Shirika limekiri mbele ya Kamati upungufu huo na limekubali kufuata ushauri wa Mdhibiti wa kupunguza gharama za kiutawala ikiwa ni pamoja na kupunguza idadi ya wafanyakazi, ingawaje zoezi hili litafanyika kwa awamu na litachukua miaka mitatu. Aidha Shirika linakusudia kufunga tawi lake la Mtwara na kupunguza wafanyakazi katika tawi la Pemba.

Maoni ya Kamati:
Kamati inaagiza kutekelezwa kwa ushauri wa Afisi ya Mdhibiti ili Shirika liweze kujiendesha kwa faida.

Wadaiwa wa Shirika (Trade Debtors):

Mdhibiti alibaini kwamba, Shirika halikuonesha wadaiwa wake wa mwaka 2007/2008 waliokuwa wakidaiwa Tsh. 57,036,411.85 na kwamba Shirika limefuta madeni ya wadaiwa hao bila ya kufuata taratibu za kisheria.

Mapitio ya Kamati.
Shirika iliandika barua kwa Wizara ya Mawasiliano na Uchukuzi pamoja na Wizara ya Fedha na Uchumi, kuhusiana na ufutwaji wa madeni hayo. Hata hivyo, Shirika halikupata majibu na hatimae kwa kupitia Bodi ya Shirika, Shirika likafuta madeni hayo.

Maoni ya Kamati:
Bado kuna tatizo la kutokufahamika kwa taratibu sahihi za ufutwaji wa madeni ya Taasisi husika. Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, kuchukuliwa hatua za makusudi za kufahamishwa hatua sahihi za ufutwaji na ufuatiliaji wa madeni ya Taasisi ya Serikali na Mashirika.Kamati imesisitiza kufuatwa kwa taratibu za kufutwa kawa madeni na haikubaliani na ufutwaji wa madeni hayo kienyeji.

24.0 SHIRIKA LA BIASHARA YA MAGARI:

Hoja namba 49.1
Matokeo baada ya Kufunga Hesabu za Mwisho wa Mwaka.

Matokeo yanaonesha wazi kwamba, Shirika lina uwezo mkubwa wa kulipa dhima zake za mpito kwa vile "current ratio" ni 2.2:1. Aidha kwa upande wa kujiendesha, Shirika linaendelea kujiendesha kwa kwa faida.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imepongeza juhudi zinazochukuliwa na Shirika na kulitaka lifanye juhudi kubwa zaidi ili liweze kupata faida zaidi.

Wadaiwa wa Shirika (Trade Debtors):
Kwa kipindi cha mwaka 2007/2008 wadaiwa wa Shirika walikuwa wakidaiwa jumla ya Tsh. 61,222,654.60. Kiwango ambacho ni kikubwa ikizingatiwa kuwa deni hili ni la mda mrefu.

Mapitio ya Kamati:
Kamati imefahamishwa kwamba madeni haya ni ya mda mredu na baadhi ya Taasisi zimeshakufa au kutokuwepo kabisa, ikiwa ni pamoja na Shirika Bizanje, Songambele, Shirika la Nyama, Matunda. Hata hivyo, Shirika limechukua juhudi mbali mbali kuendelea kudai madeni hayo ikiwa ni pamoja na kuteua baadhi ya Maofisa wake kufuatilia madeni hayo. Matarajio ya kulipwa ni madogo kwa vile baadhi ya Mashirika hudai vielelezo vya huduma (services) walizopatiwa kwa wakati huo, ambapo vielelezo hivyo haviwezi akuatikana kwa sababu huduma hizo zilitolewa muda mrefu sasa.

Maoni ya Kamati:
Kamati inashauri Serikali kupitia Wizara ya Fedha na Uchumi, kuchukuliwa hatua za makusudi kwa madeni ambayo hayawezi kulipika kutokana na kutokuwepo kwa wadaiwa hao na pia kutokuwepo vielelezo vya madeni hayo na utafutwe utaratibu wa kisheria wa kuyafuta madeni hayo. Hata hivyo, Kamati imelitaka Shirika kuorodhesha madeni yote ambayo hayalipiki na hatimae kuyawasilisha Wizara ya Fedha kwa ajili ya utaratibu wa ufutaji wa madeni kisheria.

25.0 SHIRIKA LA UTALII:

Hoja nam. 45.1 Kuhusu hati za malipo zilizokosekana kwa ukaguzi. Ukaguzi umebaini kuna fedha zimetolewa katika hesabu namba 022103000027 na 022104000560 zikiwa ni gharama za benki, lakini hati za kuthibisha uhalali wa malipo hayo hazikupatikana kwa ukaguzi.

MAPITIO YA KAMATI:
Kwa kawaida Shirika lilikua na utaratibu wa kuweka kumbu kumbu kpitia "Transfer Order" inayoamuru Benki kuhamisha pesa kutoka akaunti moja ya Shirika" na kwenda akaunti nyengine ya Shirika. Hata hivyo, baada ya kupata muongozo kwamba mbali na "Transfer Order" hiyo, pia ifanyiwe vocha, Shirika limerekebisha kasoro zilizojitokeza.

MAONI YA KAMATI:
Kwa kupitia kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inapendekeza hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 45.2 Kuhusu kitabu namba 021103000038 hakikupatikana kwa ukaguzi (Missing Receipt Book) na hatimae Afisi ya Mdhibiti imeshindwa kuthibitisha mapato yaliyokusanywa kwa kutumia kitabu hicho.

MAPITIO YA KAMATI:
Wakati wa ukaguzi kitabu namba 021103000038 hakikupatikana kwa ukaguzi hata hvyo wakati Kamati ipokuwa ikifanya kazi zake kitabu hicho kilipatikana kikiwa na na mapato hayo yamepelekwa bank kwa "pay in slip" nam:-
49457,234886,,279644,135189,108937,179439,108949,269609,136005,252184,280059,131311,257578,309544

MAONI YA KAMATI
Pamoja na kupatikana kwa kitabu hicho, Kamati imesisitiza umuhimu wa utunzaji wa kumbukumbu zote muhimu hasa zinazohuasina na mambo ya fedha.

Hoja nam. 45.3 Kuhusu malipo yaliyokosa saini za wapokeaji yenye thamani ya Tsh. 550,000/- yaliyofanywa kwa hati namba 7/3.

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli wakati wa ukaguzi, saini hizo za wapokeaji wa fedha hizo hazikuwepo. Hata hivyo, wakati Kamati inaifanyia kazi hoja hii, imeoneshwa hati hiyo ikiwa tayari imeshatiwa saini na wahusika.

MAONI YA KAMATI:
Kamati haikuridhishiwa na utendaji wa namna hiyo na kusisitiza kuwa kila malipo yanapofanyika muhisika anapaswa kusaini hapo hapo na si vyenginevyo.

Hoja nam. 45.4 Kuhusu makusanyo ya mapato ambayo hayakuingizwa katika vitabu vya fedha yenye thamani ya Tsh. 15,790,000/-

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imethibitisha kuwa wakati wa ukaguzi, makusanyo ya fedha hizo kupitia stakabadhi namba 79202 na 79143-79150 hayakuingizwa katika daftari la kuhifadhia fedha. Hata hivyo, wakati wa kazi za Kamati, tayari fedha hizo zilikwishaingizwa katika vitabu vya fedha vya Shirika na pia vimeshakaguliwa na Afisi ya Mdhibiti.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inapendekeza kufutwa kwa hoja hii.

Hoja nam. 45.5 kuhusu Malipo yasiyokuwa na Vielelezo, jumla ya USD $ 12,545, hii inatokana na vielelezo hizo havikuambatanishwa wakati wa ukaguzi.

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo hivyo vilikuwepo wakati wa ukaguzi, ingawaje Wakaguzi hawakuzikubali risiti kutoka Hoteli ya Hakuna Matata kwa sababu risiti hizo zilichapishwa kwa computer na kutiwa muhuri wa hoteli husika .

MAONI YA KAMATI:
Kwa kuwa risiti hizo zilikataliwa na Mkaguzi na Mdhibiti Mkuu wa hesabu Kamati ya P.A.C pia haikuweza kuzikubali.

Hoja nam. 45.6 Kuhusu Hati za Malipo zanye thamani ya USD 11,006 na Tsh. 2,454,312 zimekosa idhini za wasimamizi wa fedha.

MAPITIO YA KAMATI:
Maelezo ya ripoti ya Mdhibiti ni sahihi na Shirika limekiri mbele ya Kamati na kukiri kwamba tatizo hilo hivi sasa limesharekebishwa kwa wahusika hao kuweka sahihi zao ambapo hati hizo ziliwasilishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imegundua kuwa kosa hilo limefanyika kutokana na kutokuwepo kwa Mkaguzi wa ndani wa Shirika (Internal Auditor) ambaye anawajibu wa kuzikagua vocha zote kabla ya kufanyika kwa malipo.Kamati inashauri kwa upande wa mashirika kupatiwa wakaguzi wao wandani ili kuepusha makosa kama hayo.

Hoja nam 45.7 Kuhusu deni la USD $ 19,850 ambalo Shirika inaidai Royal Stars.

MAPITIO YA KAMATI:
Ni kweli Shirika halijalipwa deni hilo. Hata hivyo, Shirika limefuatilia deni hilo kisheria kwa kufungua kesi kupitia Wakili wa Kenya Ndugu Karigithu Kinyua & Advocate tarehe 19/08/2008. Hadi Kamati imepita kwa ukaguzi Shirika ilikuwa halina taarifa sahihi kuhusu maendeleo ya kesi hiyo. Aidha, Baada ya ushauri wa Kamati, Shirika limeiandikia Afisi ya Mwanansheria Mkuu wa Serikali, Zanzibar kutaka ushauri wa kesi hii kupitia barua ZTC/8/11/Vol.VI/29 ya tarehe 9/11/2009. Aidha kupitia barua ya terehe 12/11/2009 yenye kumbu kumbu L.D 21 VOL:XXXIV/7, Afisi ya Mwanansheria Mkuu pamoja na mambo mengine, ilishauri Shirika kuifuatilia kwa haraka kesi hii ambayo kwa kupitia Hati ya Madai iliyoandaliwa na Wakili huyo wa Kenya, haioneshi kupokelewa Mahakamani na hivyo kuna wasi wasi kwamba kesi hiyo haipo Mahakamani.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeshindwa kupata ukakika wa kulipwa deni hilo na kuagiza Shirika lifuatilie suala hilo kwa karibu na taarifa sahihi za maendeleo ya kesi hiyo.

Hoja namb. 45.8 Kuhusu Wadaiwa (Debtors) wa Shirika, jumla ya Tsh. 6,365,000/-.

MAPITIO YA KAMATI:
Kamati imegundua kuwa ni Tsh.1,840,000/- tu ndizo zilizolipwa.

MAONI YA KAMATI:
Kamati inaagiza madeni hayo yafuatiliwe na kuhakikisha kuwa yanalipwa.

Hoja nam. 45.9 Kuhusu Wadai wa Shirika, Tsh. 143,993,575.04.

MAPITIO YA KAMATI:
Jumla ya Tsh. 18,130,651.5 zimeshalipwa, Tsh. 104,530,793.52 hadi tunaandika ripoti hii bado fedha hizo hazijalipwa.

MAONI YA KAMATI
Kamati inasikitishwa sana na fedha zilizobaki ambazo hazijalipwa na imeagiza kutafutwa utaratibu wa kuyatafutia ufumbuzi madeni hayo.

Hoja nam. 45.10 Kuhusu malipo yasiyokuwa na vielelezo, jumla ya Tsh. 6,311,217/-

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo vilivyo kosekana wakati wa ukaguzi vililetwa mbele ya kamati na kukaguliwa .

MAONI YA KAMATI
Kamati imeagiza Shirika lirekebishe kasoro zilizojitokeza awali na kwa kutumia kifungu cha 51 (5)(c) cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 45.11 kuhusu Matokeo baada ya Kuhusu Ufungaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka shirika limfunga hesabu za miaka mine 2002/2003 hadi 2005/2006

MAPITIO YA KAMATI:
Ukaguzi umebaini kuna tafauti kubwa kati ya kumbukumbu zilizoingizwa katika vitabu vya Hesabu (Final Account) na zile kumbukumbu halisi katika daftar kuu la kumbukumbu (general ledger).Aidha idadi kubwa ya vielelezo halisi havipo kabisa na havikupatikana wakati wa ukaguzi. Hali hii imepelekea Wakaguzi kushindwa kutoa tathmini juu ya hesabu na utendaji mzima wa Shirika.Shirika limeiarifu Kamati kwamba Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu haikuliarifu Shirika kuhusu hesabu hizo ingawaje walipelekewa kwa uthibitisho na hatimae kuonekana katika ripoti hii ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeliagiza Shirika kufanya tathmini upya ya mali zake na kufunga hesabu zake vizuri pia kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali na hatimae Kamati ijuilishwe juu ya hatua iliyofikia. Aidha, Kamati haikuridhishwa na majibu ya Shirika na imeiagiza kupata taarifa sahihi baada ya Shirika kuwasiliana na Afisi ya Mdhibiti.

26.0 SHIRIKA LA BIASHARA LA TAIFA (ZSTC).

Hoja nam. 44.1 Kuhusu malipo ya Tsh. 3,697,000/- yasiyokuwa na vielelezo.

MAPITIO YA KAMATI:
Vielelezo vilivyokosekana wakati wa ukaguzi, viliwasilishwa mbele ya Kamati.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imevithibisha vielelezo hivyo, na kwa mujibu kifungu cha 51 (5) (c) cha Kanuni ya Fedha, 2005, Kamati inashauri hoja hii ifutwe.

Hoja nam. 44.2 kuhusu Uwezo wa Shirika kumudu kulipa dhima zake za muda mrefu pamoja na Uwezo wa Shirika kujiendesha kwa faida.

MAPITIO YA KAMATI:
Shirika limekiri na kutoa sababu zilizopelekea kutojiendesha kwa faida ikiwa ni pamoja na mabadiliko ya hali ya hewa, kushamiri kwa magendo ya karafuu na baadhi ya wakulima kutopeleka karafuu zao sokoni. Kuhusiana na uwezo wa Shirika kumudu kulipa dhima zake za muda mrefu, Kamati imeshauri lipunguze idadi ya wafanyakazi wake, kutoka 279 hadi 100 kwa Unguja na Pemba.

MAONI YA KAMATI:
Kamati imeshauri kufanywa marekebisho ya mfumo mzima wa utawala ili Shirika liweze kujiendesha kwa faida.

Kuhusu Utiaji wa samani za Shirika (Revaluation of Fixed Assets), Kamati imepongeza juhudi zilizochukuliwa na Uongozi wa Shirika kwa kuweka Daftari la kuhidhia mali zake na kutiwa thamani.

SEHEMU YA TATU:
HITIMISHO:

UTANGULIZI:
Kamati inapenda kutoa shukurani za dhati kwa Wizara, Idara, Mashirika na Taasisi zote za Serikali kutokana na mashirikiano makubwa walioyaonesha katika wakati wote wa kazi za Kamati. Aidha shukurani za pekee ziwafikie Afisi ya Mdhiibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mashirikiano mazuri baina yao na Kamati yaliyoipelekea Kamati kutekeleza majukumu yake kwa ufanisi.

MAMBO YALIJITOKEZA KATIKA KAZI ZA KAMATI:

- **Uwasilishaji wa Hesabu za Mwisho wa Mwaka:**

Kwa mujibu wa Sheria ya Fedha, nam 8 ya mwaka 2005, kifungu cha 24 (2) kinaeleza wajibu wa kila Taasisi ya Serikali kuwasilisha Hesabu za Mwisho wa Mwaka katika Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika kipindi cha miaka 3 baada ya kukamilika kwa mwaka wa fedha (kwa hivyo uwasilishaji usizidi tarehe 30/09/ ya kila mwaka).

Kamati imethibitishwa jumla ya Wizara na Taasisi 30 za Serikali zimecheleweshа kuwasilisha Hesabu zao za mwisho wa mwaka kwa mwaka 2007/2008. Hali hii huathiri utekelezaji mzima wa majukumu ya Afisi ya Mdhibiti. Hata hivyo, Kamati inashauri kwamba, umefika wakati wa kuchukuliwa hatua za kisheria kwa Wizara na Taasisi zote zinazochelewesha na zinazoshindwa kuwasilisha hesabu zake za Mwisho wa mwaka.

- **Kuhusu Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu (Fixed Assets Registrar).**

Kamati imeshtushwa na taarifa ya kukosekana kwa Daftari la Kuhifadhia Mali za Kudumu kwa takriban Taasisi zote za Serikali. Taarifa ilyotolewa mbele ya Kamati kwa takriban kila Taasisi iliyohusika na hoja hii ni kwamba inasubiti muongozo wa pamoja kutoka Wizara ya Fedha na Uchumi kupitia Idara ya Mhakiki Mali na Mitaji ya Umma. Kamati inasisitiza Wizara ya Fedha kuharakisha kukamilika kwa muongozo huo na kwa upande wa Taasisi husika, zinatakiwa zijiandalie utaratibu wa kuzitambua na kuzirikodi mali zake zote zinazozimiliki katika Madaftari maalum huku zikisubiri muongozo huo.

- **Madeni ya Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali:**

Ukaguzi wa Kamati umebaini kuwa katika Wizara na Taasisi mbali mbali za Serikali kuna madeni sugu nay a muda mrefu. Katika jitihada za kulitatua tatizo hili, Kamati ya P.A.C iliandaa kikao rasmi cha siku ya madeni kilichowakutanisha Wizara, Idara na Taasisi zote zenye madeni. Kamati imefikia muafaka ya suala hili kushughulikiwa kwa pamoja baina ya Wizara ya Fedha na Uchumi na Afisi ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa

Hesabu za Serikali pamoja na Afisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ili kuyatafutia utaratibu wa Kisheria wa kuyatatua madeni hayo..

- **Upotevu wa Mishahara katika Wizara na Taasisi mbali mbali :**

Kamati imeshtushwa na taarifa za upotevu wa mishahara kwa taasisi mbalimbali za Serikali. Kwa upande wa Kikosi cha Valantia, jumla ya Tsh. 23,240,556 zimepotea na kuisababishia hasara Kubwa Serikali. Aidha Tsh. 4,878,256 zimeripotiwa kupotea katika Wizara ya Afya, Pemba. Hali ya kusikitisha zaidi ni kwamba, Kamati haikupata majibu ya kuridhisha kuhusiana na upotevu huo zaidi ya taarifa kwamba, Kesi ipo Mahakamani na jambo la kusikitisha zaidi ambalo Kamati inaagiza litekelezwe mara moja, ni haki za wafanyakazi hao walioibiwa mishahara yao ambao mpaka wakati wa kuandika Ripoti hii bado hawajalipwa. Kamati inaziagiza Wizara zilizohusika kuwalipa wafanyakazi hao mara moja.

- **Kuhusiana na Uvamizi wa Mashamba ya Serikali:**

Kama ilivyoripotiwa katika ripoti ya Mdhibiti, kwa hoja namba 33.1 ya hoja husika, Kamati kwa upande wake imesikitishwa na uvamizi wa mashamba ya Serikali ambapo uvamizi huo umesababishwa zaidi na kukosekana kwa hati miliki za mashamba hayo. Aidha, kwa upande wa shamba la Makurunge liliopo Bagamoyo, Kamati imepata muda wa kulitembelea shamba hilo na kuhimiza kutafutwa kwa hati miliki ili shamba hilo liweze kuendelezwa kwa maslahi ya Zanzibar.

Hata hivyo, Kamati haikupata kufanya ziara kwa baadhi ya Mashamba ikiwa ni pamoja na Tunguu, Mpiga Duri, Maruhubi kituo cha kuogeshea mifugo na Mtoni Karakana kutokana na uchache wa muda. Kamati ina azma ya kutembelea Mashamba hayo katika kipindi kijacho cha kazi.

- **Wizi wa Kompyuta nne (4) katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali:**

Kamati imefadhaishwa na hoja ya wizi wa Kompyuta uliotokea katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na zaidi baada ya kuhoji, imefahamika wazi kwamba, juhudi za makusudi za hatua za kufuatilia wizi huo na hatimae kuwaajibisha wahusika kisheria, hazijachukuliwa ipasavyo. Kamati imefahamishwa kwamba, Afisi baada ya kutokea wizi huo ilitoa taarifa Polisi, hadi Kamati ilipofika kwa ukaguzi, hakuna hatua yoyote iliyochukuliwa kukabiliana na wizi huo. Hivyo, Kamati inashauri ikithibitika kwamba ni upotevu, Afisi ipeleke ripoti ya maandishi ya suala hili kwa Mhasibu Mkuu na Mdhibiti na Mkaguzi wa Hesabu za Serikali kwa utekelezaji kama inavyoelekezwa katika kifungu cha 22 cha Kanuni za Fedha za mwaka 2005.

- **Unuunuzi wa Samani (Furnitures) kwa Afisi ya Wilaya Ndogo ya Kojani,Pemba:**

Kamati ilifuatilia kwa karibu hoja namba 57.6 ambayo imegawika katika sehemu kuu mbili: Ya kwanza inahusu Ununuzi wa samani (furnitures) kwa ajili ya Afisi ya Wilaya ndogo ya Kojani, Pemba ambapo Tsh. 71,620,000/- zilitumika ambapo kumeripotiwa kuwepo kwa upungufu wa samani zenye thamani ya Tsh. 21,380,000/- zilizokuwa tayari zimeshalipiwa lakini hazikuonekana katika Afisi ya Wilaya Ndogo ya Kojani pamoja na kugundulika kuwa viwango vya bei vilivyotumika kwa unuzi wa samani hizo ni vya juu sana kulinganisha na samani zenyewe halisi zilizoonekana kwa ukaguzi.

Kamati inashauri suala la matumizi ya fedha za Serikali yatumike kwa kuzingatia thamani ya fedha na kitu kinachonunuliwa kama taratibu za manunuzi zinavyoelekeza.

- **Kutowasilisha fedha benki kwa Wakati:**

Kamati imegundua kuwa kuna tabia ya baadhi ya Taasisi za Serikali zinazokusanya mapato kujikopesha mapato hayo kwa matumizi ya Afisi zao bila ya kuyawasilisha Benki kwa wakati. Tatizo hili limeonekana katika Afisi ya Mrajis Mkuu wa Serikali na Idara ya Nyaraka, Makumbusho na Mambo ya Kale. Kutowasilisha fedha benki kwa wakati ni kwenda ni kwenda kinyume na kifungu 77 (1) cha kanuni za fedha 2005 Kamati inashauri kuchuliwa hatua wele wote watakao endelea na tabia ya kujikoposha fedha za mapato wanayoyakusanya.

- **Uundwaji wa Bodi kwa Taasisi zinazojitegemea:**

Kamati imegundua kuwa kuna baadhi ya Taasisi hazijiendeshi vizuri kutokana na kukosekana kwa Bodi yenye kuweza kutowa maamuzi ya namna ya uendeshaji wa Taasisi hizo. Hili limedhihirika katika Hoteli ya Bwawani kwamba pamoja na kasoro ndogo ndogo zilizojitokeza, Uongozi wa Hoteli unashindwa kuiendeleza Hoteli ipasavyo kutokana na kukosa chombo chenye uwezo wa kushauri ipasavyo na kutoa maamuzi ya haraka na fanisi. Hivyo, Kamati inashauri kwa zile Taasisi za Serikali zinazojitegemea na zenye muundo wa kibiashara mfano Hoteli hii ianzishe Bodi yake.

- **Udhaifu katika Udhibiti wa ndani.**

Vile vile imegundulika kwamba, kukosekana kwa Udhibiti wa ndani na kukosekana kwa Mkaguzi wa ndani anaeshughulikia Taasisi husika ni tatizo kubwa linalopelekea upetevu wa fedha za Serikali. Kwa mfano, katika Hoteli ya Bwawani bado matatizo haya yanaendelea. Kwa upande wa Shirika la Huduma za Maktaba, Kamati imeshtushwa na upotevu wa Tsh. 26,963,500/- katika Shirika hili liliosababishwa zaidi na aliyekuwa Mhasibu wa Shirika hilo kwa wakai huo ambae yeye yeye ndie Mhasibu, Mkaguzi wa ndani na Mshika fedha. Kamati kwa upande wake inashauri kwa kutumia kifungu cha 51 (5) (a) cha Kanunuzi za Fedha, 2005 kuchukuliwa hatua za kinidhani kwa muhusika huyu popote alipo.